

Maswali

1. Mamajusi waliona nini?
2. Walifuata nyota wakienda mji gani?
3. Mamajusi waliuliza watu wa Yerusalemu nini?
4. Mbona Herode alikasirika?
5. Wakuu wa Makuhani walisema kwamba Yesu atazaliwa wapi?
6. Mfalme Herode alitaka mamajusi wafanye nini?
7. Mamajusi walimpa Yesu zawadi gani?
8. Malaika aliambia mamajusi nini?
9. Malaika aliambia Yusufu nini kwa ndoto?
10. Mariamu na Yusufu walipeleka Yesu wapi kumwoko?

Majibu

1. Mamajusi waliona nyota isiyo ya kawaida.
2. Walifuata nyota mpaka Yerusalemu.
3. Waliuliza, "Wapi mtoto aliyezaliwa kuwa Mfalme wa Wayahudi?"
4. Herode hakufurahia kwa sababu mamajusi walisema kulikuwa na mfalme mwingine kando yake. Aliua mtu yeyote aliyemdhania kuwa ni mfalme.
5. Wakuu wa Makuhani walisema kwamba Mfalme angezaliwa Bethlehemu.
6. Warudi na wamwambia penye mtoto ako.
7. Mamajusi walipea Yesu dhahabu, uvumba na manemane.
8. Mfalme Herode alitaka kumuua Yesu, kwa hivyo warudi nyumbani kwa njia ingine.
9. Kwamba Mfalme Herode alitaka kumuua Yesu kwa hivyo watoroke.
10. Mariamu na Yusufu walimpeleka Yesu Misri.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 3

37 Mamajusi wanaenda kuona Yesu

Marejeo

Mathayo 2: 1 – 18

Kiini cha somo

Kuonyesha imani kuu ya Mamajusi waliosafiri mwendo mrefu kwenda kumuona Yesu.

Maneno maalum

- 37.1 Mamajusi + Mashariki + nyota isiyo ya kawaida + Mfalme wa ajabu kazaliwa + fuata nyota + Yerusalemu + wapi mtoto Mfalme?
- 37.2 Mfalme Herode + muovu + kasirika + Makuhani Wakuu + Bethlehemu + rudi mniambie
- 37.3 Mamajusi + Bethlehemu + Yesu + zawadi + malaika + Herode + panga kuu + rudi nyumbani kwa njia nyingine
- 37.4 Yusufu na Mariamu + malaika + Herode apanga kuu Yesu + toroka + Misri + Yesu ameokoka

37.1 Mamajusi kutoka mashariki waliona nyota isiyo ya kawaida. Walijua kwamba ni ishara ya kuonyesha mfalme mkuu amezaliwa. Walifuata nyota ili wampate mtoto mfalme na wampe zawadi. Labda walitumia ngamia wakibeba zawadi nzuri kupelekea mtoto mfalme aliyezaliwa. Mamajusi walisafiri wakaenda kwa nchi ya Israeli, kwa mji wa Yerusalemu kumtafuta mfalme mpya.

Mamajusi walipofika Yerusalemu, waliuliza watu, “Wapi mtoto aliyezaliwa kuwa mfalme wa Wayahudi? Tumeona nyota yake mashariki na tumekuja kumsujudia.”

37.2 Mfalme Herode aliishi Yerusalemu kwa nyumba ya kifalme. Alikuwa mfalme katili na muovu. Aliua kila mtu aliyemfikiria kwamba anataka kuwa mfalme. Watu waliogopa waliposikia mamajusi wakitafuta mfalme mwingine. Herode angekuwa na hasira aje! Mamajusi walienda mpaka kwa nyumba ya kifalme ili wamuulize Mfalme Herode ni wapi mtoto mfalme amezaliwa. Mfalme Herode alikasirika sana alipoulizwa na mamajusi juu ya mfalme mpya aliyezaliwa, lakini alijifanya kama hajakasirika.

Mfalme Herode aliwauliza juu ya nyota waliyofuata kutoka Mashariki. Walimwambia juu ya nyota na safari yao kuja Israeli ili wamwone mfalme mpya. Mfalme Herode alijua kwamba Wayahudi walitumainia Mfalme wa kuwaokoa, kwa hivyo alituma waite Makuhani Wakuu ili awaulize ni wapi Mfalme atazaliwa. Wakuu wa Makuhani walikuwa wamesoma Biblia, walisema, “Nabii alisema kwamba Mfalme atazaliwa Bethlehemu.” Mfalme Herode aliwambia waende Bethlehemu, wamwone mtoto halafu wakuje wamwambie penye ako. Mfalme aliwambia Mamajusi kwamba naye alitaka kwenda kumsujudia, lakini ukweli ni kwamba alitaka KUMUUA Yesu.

37.3 Mamajusi walishukuru Mfalme Herode na kuendelea na safari ya kwenda Bethlehemu. Kule walimpata Yesu. Walipofika kwa nyumba walimkuta mtoto Yesu pamoja na mamaye Mariamu. Waliinama chini na kumsujudia. Walimpa zawadi – dhahabu, uvumba na manemane.



Huko Herode aliongoja mamajusi warudi wamwambia penye mtoto anaishi. Alipanga kumuua huyu mtoto aliyezaliwa kuwa Mfalme. Lakini Mungu alikuwa akimlinda Yesu, na akawambia hao mamajusi wasirudi kwa Herode kwa sababu alipanga kuuu Yesu. Kwa hivyo mamajusi walirudi nyumbani kwao kutumia njia ingine.

37.4 Yusufu na Mariamu hawakujua hatari iliyokuweco kwao. Siku moja malaika alikuja Yusufu kwa ndoto. Akamwambia, “Enuka, chukua mtoto na mama yake halafu mtorokee Misri kwa sababu Herode anataka kumuua.” Yusufu aliamka kwa giza ya usiku huo na kutoroka pamoja na Mariamu na Yesu wakaenda Misri.

Mapema asubuhi moja, baada ya Yusufu kuondoka, maaskari wa Herode walizunguka Bethlehemu. Herode alikuwa amepeana amri mbaya kwamba askari waue watoto wote Bethlehemu waliokuwa na umri wa miaka mbili kurudi chini. Mpango mbaya wa Herode haungefaulu kumuumiza Yesu kwa sababu Yesu alikuja kuokoa ulimwengu.